

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA NANE

11 NOVEMBA, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO


KIKAO CHA NANE – TAREHE 11 NOVEMBA, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021*].



MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2021 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021*].

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

79. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwahamasisha Vijana kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

80. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa kipaumbele kwa kuongeza mtandao wa barabara za lami za Mji mkongwe na wa kitalii wa Mbamba Bay.

**81. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO
(SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, mpango wa kuzipandisha hadhi Sekondari za Ngweli, Ngoma A, Tamabu, Nyamatongo, Sima, Nyampande na Katunguru kuwa za Kidato cha Tano na Sita Wilayani Sengerema umefikia wapi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**82. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO
MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni Ranchi ngapi nchini zimeshawapokea Wafugaji na kuwapatia nafasi ya kufuga kwenye Ranchi hizo kama Serikali ilivyotoa maelekezo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

83. MHESHIMIWA MOHAMMED JUMAH SOUD (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani ya kupunguza au kuondosha kabisa wizi wa mazao ya kilimo na mifugo katika maeneo ya Unguja na Pemba.

84. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutenganisha Mahabusu/Magereza ya Watoto na Watu wazima ili kuwalinda Watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kingono vinavyoweza kujitokeza.

WIZARA YA MAJI:

**85. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA
HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kuendeleza mradi wa maji wa Lukululu ili kumaliza tatizo la maji katika Vijiji 14 vya Jimbo la Vwawa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**86. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE
NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi barabara ya Igumbi – Mbutu – Igunga hadi Itumba yenye zaidi ya km 140 kuwa chini ya TANROADS ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

**87. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA
(MTAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha uwepo wa Marubani wawili kwenye Ndege ndogo za abiria.

**88. MHESHIMIWA JOSEPH KASHEKU
MUSUKUMA (GEITA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa kilometa 20 kutoka Nkome hadi Nzera.



V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***[Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima
na Kusomwa Mara ya Tatu]***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021]*.

**DODOMA
11 NOVEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**